

Dai Pesa Zako



Huenda unastahili kupata hadi **\$6,000** au zaidi katika rudisho yako ya ushuru unapodai **Rudisho ya Ushuru wa Kazi (Earned Income Tax Credit)** na **Rudisho ya Ushuru kwa Watoto (Child Tax Credit)**

1

Pata sehemu ya BURE ya ushuru*

Tazama irs.treasury.gov/freetaxprep au piga simu **800-906-9887**.

2

Angalia kama unastahili

Tambymuch unaweza kupokea katika eitcoutreach.org/help.

3

Jaza fomu zako za ushuru

Tembelea mahali pa bure kufikia Aprili 18 ujaze fomu zako za ushuru na upokee pesa zako katika rudisho ya ushuru.

*Bado unaweza kudai rudisho za ushuru (tax credits) hata kama huwezi kupata mahali pa ushuru bila malipo karibu yako.

Lini utajaza fomu zako za ushuru?

Tarehe:

Saa:

Mahali:

Simu:

Kwa maelezo zaidi, tazama eitcoutreach.org/help au pigia simu IRS kwa **1-800-829-1040**.

GET IT
BACK

SW

JE, NASTAHILI?

Rudisho ya Ushuru wa Kazi (Earned Income Tax Credit) na Rudisho ya Ushuru kwa Watoto (Child Tax Credit) ni mafao ya ushuru kwa watu wanaofanya kazi. Huenda utadaiwa ushuru wa chini zaidi na urudishiwe pesa taslimu!

Kudai rudisho hizi hakutaathiri kustahili kwako kwa mafao kama SNAP (stampu za chakula), SSI, Medicaid, usaidizi wa fedha, au nyumba za jamii. Rudisho zinazowekwa akaunti ya akiba hazihesabiwi dhidi ya viwango vya programu/taasisi za usaidizi zinazodhaminiwa na serikali miezi 12 baada ya rudisho kupokewa.

KAMA UNA WATOTO

- Umri:** Kwa EITC, watoto lazima wawe na umri usiozidi miaka 19 mwisho wa 2016 (wanaosoma muhula mzima wanaweza wasizidi miaka 24 na watoto wenye kilema kiasi au kamili wanaweza kuwa wa umri wowote). Kwa CTC, watoto lazima wawe na umri usiozidi miaka 17 mwisho wa 2016.
- Makao:** Watoto lazima wawe wameishi nawe kwa zaidi ya nusu ya 2016.
- Mapato ya 2016:** Kwa CTC, kama ulipokea zaidi ya \$3,000, unaweza kudai hadi \$1,000 kwa kila mtoto.

Kwa EITC, mapato yako lazima yawe chini ya viwango vifwatavyo:

Watoto	Haujafunga ndoa	Umefunga ndoa	EITC hadi:
1	\$39,296	\$44,846	\$3,373
2	\$44,648	\$50,198	\$5,572
3 au zaidi	\$47,955	\$53,505	\$6,269

Nini unastahili kuleta katika mahali pa ushuru bila malipo

- Kitambulisho halali chenye picha
- Kadi ya Hazina ya Jamii (Social Security Number), barua ya thibitisho la kuwa na Social Security Number, au ITIN
- Fomu za W-2 au 1099
- Thibitisho la bima ya afya (Fomu za 1095-A, 1095-B, au 1095-C)

KAMA HAUNA WATOTO

- Umri:** Lazima uwe na umri wa kati ya miaka 25 na 64.
- Mapato ya 2016:** Kama ulipokea mapato yasiyozidi \$14,880 (\$20,430 kama umeowa/umeolewa), unaweza kupokea hela za EITC hadi \$506.

KAMA WEWE SI MWANANCHI

- EITC:** Wewe, mume/mke wako, na mtoto yeyote unaemshughulikia lazima muwe na Namba halali ya Hazina ya Jamii (Social Security Number).
- CTC:** Wewe, mume/mke wako, na mtoto yeyote unadai lazima muwe na Hazina ya Jamii (Social Security Number) au Namba ya Binafsi ya Kujitambua (Individual Taxpayer Identification Number, ITIN).

Bima ya Afya

Kama hauna bima ya afya, Mpango wa Ushuru wa Premium Tax Credit itaweza kulipia gharama kubwa ya mpango wa afya! Jiandikishe kati ya Nov. 1, 2016 na Jan. 31, 2017. Baadhi ya watu wasiokuwa na bima huenda watatozwa ada. Pata maelezo zaidi kwa

1-800-318-2596 au **www.HealthCare.gov**.